



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA AFYA**

**MAMLAKA YA DAWA NA VIFAA TIBA**

**TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA KUFUATILIA UBORA WA DAWA  
KATIKA SOKO KWA MWAKA WA FEDHA 2021 – 2022**

**KANDA YA MASHARIKI**

Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba, TMDA Kanda ya Mashariki  
P. O. Box 31356, Jengo la Victoria, Barabara ya Ali Hassan Mwinyi, Dar es Salaam  
Tel: +255-737-226328/788470301, Fax: +255-22-2450793  
Website: [www.tmda.go.tz](http://www.tmda.go.tz), Email: [info.eastzone@tmda.go.tz](mailto:info.eastzone@tmda.go.tz)

## 1.0 UTANGULIZI

Mfumo wa kufuatilia ubora wa dawa katika soko (PMS), ni utaratibu uliowekwa kwa lengo la kuhakiisha kuwa dawa zilizopo katika soko zinaendelea kukidhi vigezo vilivyoidhinishwa wakati wa usajili.

Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) hutumia njia kuu mbili kufuatilia ubora wa dawa katika soko ikiwa ni pamoja na mpango maalumu wa kufanya uchunguzi wa awali (screening) wa sampuli za dawa kwa makundi yaliyochaguliwa kwa kuchukua sampuli katika vituo vya forodha, Bohari ya Dawa na viwanda vya ndani pamoja na mpango wa kila miaka mitatu wa kufuatilia ubora wa dawa katika soko (structured PMS program) unaoandaliwa kwa kuzingatia vihatarishi katika usambazaji na matumizi ya dawa husika.

Majukumu ya ofisi za kanda katika kutekeleza mipango hii ni kukusanya sampuli na kufanya uchunguzi wa awali kwa kutumia maabara hamishika (Mini lab).

Kanda ya Mashariki ina jumla ya maabara hamishika tatu ambapo mbili zipo Mkoa wa Tanga na moja Dar es Salaam.

Katika mwaka wa fedha 2021/22 kanda ya Mashariki imetekeleza kazi hizo kama zilivyokuwa zimepangwa.

### 1.1 LENGU KUU

Lengo la mfumo huu (PMS) ni kuhakikisha dawa zinaendelea kukidhi vigezo vya ubora, usalama na ufanisi kama vilivyoidhinishwa wakati wa usajili.

### 1.2 MBINU ZILIZOTUMIKA

Sampuli za dawa za kufubaza makali ya Virusi Vya Ukimwi, kutibu Kifua Kikuu na Malaria zilikusanywa kutoka katika vituo vya forodha, Bohari ya Dawa (MSD) na viwanda vya ndani. Sampuli husika zilifanyiwa uchunguzi wa awali katika maabara hamishika zilizopo ofisi ya Kanda ya Mashariki. Aidha, katika kutekeleza mpango wa kufuatilia ubora wa dawa katika soko (Structured PMS program 2021/22), sampuli zilikusanywa kutoka katika maeneo mbalimbali (Hospitali, Bohari ya Dawa, waagizaji binafsi, maduka ya dawa jumla na rejareja) kwa kuzingatia mpango wa kuchukua sampuli uliowasilishwa (sampling plan).

## 3.0 MATOKEO YA UTEKELEZAJI

### 3.1 Mpango maalum wa kufuatilia ubora wa makundi ya dawa (ARVs, Anti-TB na Anti-Malarials) yaliyochaguliwa

Jumla ya sampuli 646 zilikusanywa na kufanyiwa uchunguzi wa awali (screening) kama ilivyoainishwa katika jedwali lifuatalo.


#### Jedwali Na 1: Idadi ya sampuli zilizokusanywa kwa makundi ya dawa

Na	Kundi la dawa	Idadi ya sampuli	Zilizokidhi vigezo	Asilimia (%)
1	ARVs	136	136	100%
2	Anti-Malarials	470	470	100%
3	Anti-TB	10	10	100%
4	Antibiotics	30	30	100%

<b>Jumla</b>	<b>646</b>	<b>646</b>	<b>100%</b>
--------------	------------	------------	-------------

### 3.2 Uwiano wa sampuli za dawa zilizokusanywa

Uwiano wa sampuli zilizokusanywa kwa makundi ya dawa umeainishwa katika mchoro namba 1 hapa chini.



### Mchoro Na 1: Uwiano wa sampuli zilizokusanywa kwa makundi ya dawa

### 3.3 Sampuli zilizokusanywa katika kutekeleza awamu ya III&IV ya mpango wa kufuatilia ubora wa dawa (PMS Program 2021/22)

Jumla ya sampuli 67 za dawa za binadamu zilikusanywa katika kutekeleza awamu ya III & IV mpango wa kufuatilia ubora wa dawa katika soko kama zilizyoainishwa katika jedwali namba 2 hapa chini.

Sampuli husika zinafanyiwa mapitio ya taarifa (Product information review) na uchunguzi wa maabara kisha taarifa kamili kuandaliwa na kusambazwa kwa umma.

### Jedwali Na 2: Sampuli zilizokusanywa katika kutekeleza awamu ya III & IV ya mpango wa kufuatilia ubora wa dawa.

Na	Jina la dawa	Dosage form	Idadi ya sampuli
1	Ampicillin 250 mg + Cloxacillin 250 mg	Kapsuli	22
2	Albendazole 200 mg	Vidonge	23
3	Sulfamethoxazole 400 mg + Trimethoprim 80 mg	Vidonge	22
<b>Jumla</b>			<b>67</b>

### 4.0 Muono mbele (Way forward)

TMDA Kanda ya Mashariki inaendelea kutekeleza kazi ya kufuatilia ubora wa dawa kwa kukusanya sampuli toka katika vituo vya forodha, Bohari ya Dawa na viwanda

vya ndani. Aidha, uchunguzi wa sampuli zilizotumwa kwenda Kurugenzi ya Udhhibiti wa Dawa za Binadamu na Mifugo unaendelea.

**IMEANDALIWA NA TMDA KANDA YA MASHARIKI**



**A. A. BITEGEKO  
MENEJA WA KANDA**